



## Makubaliano ya Kuripoti Mabadiliko

*Makubaliano haya yanahusiana na mafao yafuatayo: 3SquaresVT, Fuel Assistance, Reach First, Reach Up, Reach Ahead, Essential Person, na Postsecondary Education (PSE).*

### **Nikipata (au ikiwa nimetuma maombi ya) mafao ya 3SquaresVT:**

Ninastahiki Kutoa Taarifa Kulikorahisishwa na lazima nitoe taarifa ndani ya siku 10 baada ya mwezi ambao jambo lolote kati ya yafuatayo litatokea:

- Mapato ya familia yangu yakifika 130% ya kiwango cha umaskini cha serikali kuu (tazama Jedwali la Mapato ya Jumla ya 3SquaresVT sehemu ya nyuma); au
- Saa za kazi kwa wateja wenye ukomo wa muda zinapopunguzwa hadi chini ya saa 20 kwa wiki/saa 80 kwa mwezi.

### **Nikipata (au ikiwa nimetuma maombi ya) mafao ya 3SquaresVT PEKEE:**

Ninastahiki Kutoa Taarifa Kulikorahisishwa. Tazama masharti ya kutoa taarifa hapo juu.

### **Nikipata (au ikiwa nimetuma maombi ya) mafao yoyote kati ya yaliyoorodheshwa hapo juu (bila kujumuisha 3SquaresVT):**

Lazima kutoa taarifa ndani ya siku 10 mabadiliko yafuatayo katika kaya yangu:

- Hali ya maisha: ninapoishi, anwani yangu, watu wanaoishi nami, jinsi nyumbani kwangu kunavyopashwa joto au anayesambaza mafuta ya kupasha joto nyumbani kwangu.
- Mapato: kuongezeka au kupungua kwa mapato kutoka kwenye chanzo chochote: ajira mpya au kupoteza ajira, vyanzo vipya vya mapato, ufadhili wa mtoto, ruzuku ya serikali, pensheni, fidia ya kukosa ajira, fedha za ushindi wa bahati nasibu au bingo, malipo ya jumla, urithi, au malipo ya bima.
- Gharama (bila kujumuisha Reach Ahead na Fuel Assistance): gharama binafsi za matunzo ya mtoto au mtu mzima anayekutegemea au malipo ya ufadhili wa mtoto.
- Rasilimali (bila kujumuisha Reach Ahead na Fuel Assistance): akiba, mali au magari.
- Mabadiliko mengine: pale mtu katika kaya yangu anapokuwa na mtoto au anapoa/kuolewa.

### **Nikipata (au ikiwa nimetuma maombi ya) Reach First, Reach Up, Reach Ahead, au Postsecondary Education:**

Lazima pia kutoa taarifa wakati:

- Mzazi wa mtoto wangu anarudi nyumbani kwangu, au pale mabadiliko ya hali yake yanamwathiri mtoto wangu.
- Kodi yangu ya nyumba au gharama nyingine za nyumba zinabadilika (bila kujumuisha Reach Ahead).
- Pesa taslimu, hisa, hati na pesa za familia zilizo benki jumla ni \$9,000 au zaidi (bila kujumuisha Reach Ahead).

### **Ninaelewa kwamba:**

- ✦ Kwa kusaini maombi haya, ninaapa kwa mujibu wa adhabu ya kusema uwongo kwamba taarifa zilizotolewa katika maombi haya ni sahihi na kamili kadri ya ufahamu na imani yangu. Pia nimesoma na kuelewa Haki na Wajibu katika maombi na ninayakubali.
- ✦ Lazima nitoe taarifa kwenye Idara ya Watoto na Familia, Kitengo cha Huduma za Uchumi (Department for Children and Families, Economic Services Division (ESD)) kuhusu mabadiliko ya hali yangu wakati ulioelezwa hapo juu.
- ✦ Ninaweza kuripoti mabadiliko kwa kuwasiliana na Kituo cha Huduma ya Mafao (Benefit Service Center) kwa namba 1-800-479-6151 au kwa kutuma Fomu ya Ripoti ya Mabadiliko au taarifa ya maandishi kwenda Application and Document Processing Center (andika anwani upande wa nyuma).
- ✦ Lazima niwasiliane na ESD kama nina shaka lolote kuhusu aina ya taarifa za kuripoti.
- ✦ Ninaelewa kwamba nikipokea fidia za Reach First, Reach Up, Reach Ahead, PSE, Fuel, au 3SquaresVT ambazo hazinihusu, ninaweza kutarajiwa kuzilipa.
- ✦ Ninaweza kushtakiwa kwa udanganyifu au kuwekewa vikwazo vingine vya kiutawala, nikikiuka sheria hizi.

**Tazama Jedwali la Mapato ya Jumla ya 3SquaresVT sehemu ya nyuma.**

**Tafadhali hifadhi taarifa hizi kwa ajili ya kumbukumbu zako.**

## Jedwali la Mapato ya Jumla ya 3SquaresVT

Kwenye safu ya upande wa kushoto wa Jedwali chini, utaona idadi ya watu walio kwenye 3SquaresVT katika kaya yako. Lazima utoe taarifa ESD, kama ulivyoelekezwa kwenye ukurasa wa mbele, ikiwa mapato ya kaya yako yatazidi kiasi hiki.

Mapato yanajumuisha mishahara, ajira binafsi, hifadhi ya jamii, fidia ya kukosa ajira, msaada wa mtoto, pensheni, fedha za bahati nasibu au bingo, malipo kwa jumla, urithi au malipo ya bima. "Jumla" inamaanisha kabla ya kutozwa ushuru.

Ili kutoa taarifa mabadiliko, unaweza kuwasiliana na Kituo cha Huduma za Mafao kwa namba 1-800-479-6151, au tuma taarifa ya maandishi au fomu ya Taarifa ya Mabadiliko kwenda:

**DCF – Economic Services Division**  
**Application and Document Processing Center**  
**280 State Drive**  
**Waterbury, VT 05671-1500**

Unaweza kupata Fomu ya Kutoa Taarifa ya Mabadiliko kwa kupiga simu 1-800-479-6151, au kwa kutembelea [myBenefits.vt.gov](http://myBenefits.vt.gov) ili uichapishe.

<b>Ukubwa wa Kaya</b>	<b>Mapato ya Kila Mwezi ya Jumla ya Juu Zaidi 130% ya Kiwango cha Umaskini</b>
1	\$1,580.00
2	\$2,137.00
3	\$2,694.00
4	\$3,250.00
5	\$3,807.00
6	\$4,364.00
7	\$4,921.00
8	\$5,478.00
9	\$6,035.00
10	\$6,592.00

<b>Kila Mwanafamilia wa Ziada</b>	<b>Ongeza \$557.00</b>
-----------------------------------	------------------------